Pastor James Kalekwa



# MAPENZI YA MUNGU KUHUSU MAPENZI

# MAPENZI YA MUNGU KUHUSU MAPENZI.

# Orodha ya Yaliyomo:


**Orodha ya Yaliyomo:** ........................................................ 3

**Tabaruku** ........................................................ 4

**Salamu na Utangulizi** ........................................................ 5

**NENO LA UTANGULIZI** ........................................................ 7

**SURA YA KWANZA:** ........................................................ 9

**USULI WA FUNDISHO LA KITABU HIKI.** ........................................ 9

**SURA YA PILI:** ........................................................ 12

**HOMA YA KUMPATA MTU SAHIHI** .................................... 12

**SURA YA TATU: NAMNA YA KUANZISHA MAHUSIANO.** ..... 43

- **Namna ya kuwa mtu sahihi** ........................................ 44
- **Wewe ni nani** ........................................................ 47
- **Wapi pa kutafuta** ........................................................ 49
- **Sehemu ya kupata mwenzi** ........................................ 51

**SURA YA NNE: UMRI WA KUINGIA KWENYE MAHUSIANO** 54

- **Kuitambua dhahabu katikati ya mchanga** ...................... 59

**SURA YA TANO: NAMNA YA KUENDESHA MAHUSIANO** .... 72

**Kuhusu Mwandishi:** ........................................................ 77

**Kuhusu New Vine Church:** ........................................ 77

**Mawasiliano na Mwandishi:** ........................................ 78

# Tabaruku

Mfululizo wa vitabu hivi vya kieltroniki (e-books) bure kwa kila atakaye; ni himizo la kiungu ndani yangu kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari.

Ninatabaruku kitabu hiki kwa kanisa la Kristo na kwa nchi yangu niipendayo, Tanzania.

Kanisa litashinda na kushamiri zaidi!

Tanzania, ninakupenda kwa moyo wote!

# Salamu na Utangulizi

Mfululizo huu wa vitabu vya kieletroniki ni maono ambayo Mungu ameweka ndani ya mtumishi wake, mume wangu mpenzi, kama namna yake ya kuonyesha shukurani kwa Mungu kwa zawadi ya maisha.

Ninamfahamu mume wangu kama mtu anayempenda Mungu kupitiliza. Yuko tayari kulipia gharama yoyote ile kuonyesha hilo. Ni mtu anayewapenda watu wa Mungu kwa namna ambayo sijawahi kuona. Yamekuwa ni maombi yake kuyagusa maisha ya wengi kwa kadiri inavyowezekana kabla Yesu Kristo hajarudi.

Anapoadhimisha siku ya kuzaliwa kwake **Juni 20**, amekuandikia kitabu hiki, akapangilia na kufanya kipatikane kwako bila malipo yoyote. Nimemwona anavyokesha; wakati mwingine kuamka alfajiri sana au kuchelewa sana kulala ili kukamilisha uandishi. Nimemuona anavyoomba na kuombea wasomaji, anavyojisomea na kutafiti ili kuhakikisha anafanya uwasilishaji wa thamani.

Ningependa tuthamini zawadi hii ambayo sisi wengine tunanufaika nayo bila kulipia gharama:

1. Mshukuru Mungu pamoja nasi kwa zawadi hii ya maisha ya Pastor James Kalekwa kisha muombee maisha marefu na afya njema.

2. Mwandikie ujumbe wa kumsalimu na kumpongeza ukisema ni kwa namna gani huduma yake imeyagusa maisha yako. Ninajua hili litaufurahisha sana moyo wake.

3. Wafikishie vitabu hivi walau watu hamsini tu. Ni vitabu vinatolewa bila malipo (vimeyagharimu maisha ya mwandishi ili vikufikie).

4. Usiuze vitabu hivi. Tuligundua kuwa kuna watu wanavisambaza kwa malipo ya fedha. Hiyo si sawa. Itakuwa ni kwa hasara yako mwenyewe ukifanya hivyo.

Baada ya kuyasema hayo, nikuhakikishie ya kwamba mtu huyu mkuu wa Mungu amejaa hekima za kiungu na neno ambalo siku zote hutokeza shuhuda maishani mwa wengi. Kwa kusoma kitabu hiki, ushuhuda wako unafuatia. Nikutakie usomaji mwema.

Na heri ya kuzaliwa kwa mpendwa wetu, zawadi ya mbingu kwenye kizazi chetu, Pastor JK.

Frida James Kalekwa (Mama Pastor JK)

Mke wa mwandishi

Juni, 2024

Dodoma, Tanzan

# NENO LA UTANGULIZI

Wim 3:7 “Nawasihi, enyi binti za Yerusalemu, kwa paa na kwa ayala wa porini, msiyachochee mapenzi wala kuyaamsha, hata yatakapoona vyema yenyewe”

Wim 3:5 “Nawasihi, enyi binti za Yerusalemu, kwa paa na kwa ayala wa porini, msiyachochee mapenzi wala kuyaamsha, hata yatakapoona vyema yenyewe”

na Wim 8:4 “Nawasihi, enyi binti za Yerusalem, kwani kuyachochea mapenzi,au kuyaamsha, Hata yatakapoona vema?”.

Je unadhani ni kwa bahati mbaya wosia na hekima hii kutolewa kwa vijana mara 3 ndani ya kitabu kimoja? Kama ilivyo usingizi ni zawadi njema kutoka kwa Mungu, kama yasemavyo maandiko, “Kila kitu amekifanya kizuri kwa wakati wake…” Mhubiri 3:11 ndivyo kuna ufahamu na sanaa ya kumwamsha mtu kutoka usingizini, ama sivyo madhara yake ni makubwa, ndivyo yalivyo mapenzi, zawadi kutoka kwa Mungu, kuna ufahamu na sanaa ya kuyaamsha. Na sanaa hiyo ya kuyamsha mapenzi inapatikana ndani ya neno la Kristo.

Nakukaribisha kusoma kitabu hiki kinachoitwa "MAPENZI YA MUNGU KUHUSU MAPENZI" na kutokea kwenye kitabu hiki ninaamini kuwa utapokea hekima zitakazoyapa maisha yako thamani. Iwe amani, utele na utoshelevu kwako, Shalom!

# SURA YA KWANZA:

# USULI WA FUNDISHO LA KITABU HIKI.

Kila unapokuja msimu wa kuelekea siku ya valentine (siku ya wapendanao) kumekuwa na sauti nyingi zikizungumza kuhusiana na upendo, mapenzi, ndoa na uchumba. Kuna semina nyingi sana zinaandaliwa hukusiana na vitu hivi, kumekuwa na sauti redioni, kwenye mitandao ya kijamii pamoja na kanisani; japokuwa kanisani sauti huwa ni ya chini sana. Kumekuwa na sauti kutoka kwa watu tunaowaamini na tusio waamini. Ninajua kwenye nafasi uliyopo kuna taarifa nyingi sana ulizonazo kuhusiana na mahusiano. Katikati ya sauti hizo nyingi mimi kama mchungaji wa vijana nimekutana na maswali mengi kutoka kwa vijana, swali kuu likiwa "tufuate sauti gani?"

Katikati ya hizo kelele vijana wanachanganyikiwa, na kuchanganyikiwa huko mara nyingi hawasemi hadharani. Vijana wana changamoto kubwa katika hilo eneo; wakijifungia chumbani ndipo wanaanza kujiuliza sauti ipi ni sahihi. Dunia nayo inapiga kelele kwa sauti sana

kuhusiana na mambo ya mahusiano, ndoa, mapenzi na uchumba mpaka kanisa tumekuwa tukiisema kwa ukimya.

Kitabu hiki siyo moja ya hizo sauti, kitabu hiki siyo kwa vile kuna siku ya valentino ndiyo maana nimeandika kitabu hiki, hapana! Hiki ni kitabu chenye sauti yenye mamlaka. Nimesoma sana vitabu, nimesoma vitabu ya watu wa falsafa, nimesoma vitabu vya watu wa saikolojia lakini pamoja na kusoma kwangu vitabu vyote hivyo sijawahi kukutana na kitabu kilichojaa kweli za maisha kama Biblia. Chochote unachohitaji maishani kipo kwenye kitabu kinaitwa Biblia. Biblia hii inatufundisha pia kuhusiana na mahusiano.

Nitawekeza muda sana kuzungumzia kuhusu upendo, mapenzi na ndoa; na haya maarifa ni lazima yatakusaidia kwa wakati huu uliopo au siku za mbeleni, kwahiyo ni muhimu sana kuyazingatia. Pamoja na maswali mengi ambayo yatajibiwa na neno la Mungu ndani ya kitabu hiki, lakini kuna maswali matatu ambayo nimeyaleta kwa nguvu ili tuweze kuyajibu kama ifuatavyo:

i. Swali la kwanza: Homa ya kumpata mtu sahihi "The right person syndrome". Vijana wengi wanajiuliza maswali kama: Nitajuaje mtu sahihi? Nitajuaje ametoka kwa Bwana? Nitajuaje huyu ndio Mungu anataka niolewe naye au nimuoe? Nitajuaje ya kwamba huyu ndiye ambaye ametoka kwenye moyo wa Bwana. Vilevile, kuna vijana wengine walienda mbele zaidi na kuniuliza wakisema; Vipi nikigundua ya kwamba huyu mtu siyo sahihi je naweza nikamuacha nikatafuta mtu sahihi? Ndio maana nikaita ni "homa" kwa maana ya kwamba ni ugonjwa. Vilevile namna ya kumtambua au kumpata huyo mtu sahihi, je niombe? Nifunge? Sasa, nataka kuvunja hiyo homa ya kwamba homa ya kumpata mtu sahihi sio sahihi.

ii. Swali la pili: Umri wa kuanza mahusiano: Umri gani ni sahihi wa kuanza mahusiano? Ni lini na ni wakati gani wa kuwa kwenye mahusiano.

iii. Swali la tatu: Namna ya kuendesha hayo mahusiano.

# SURA YA PILI:

# HOMA YA KUMPATA MTU SAHIHI

Swali tunalojiuliza ni Je, Mungu huchagua wenzi kwa ajili yetu? (Je, Mungu anatuchagulia?). Kuna ushahidi wa kimaandiko mwingi wa namna Mungu aliwachagulia watu wenzi wa maisha yao. Kwenye mazingira gani Mungu aliwachagulia watu wenzi, na sio tu aliwachagulia, aliwalazimisha waolewe na waoe wenzi hao (kuna ushahidi wa kimaandiko). Lakini kuna sababu nyuma yake kwanini Mungu alifanya hivyo. Je sisi tupo kwenye uhitaji huo ili Mungu ama atuchagulie au atulazimishie.

Lakini pia kuna ushahidi wa kimaandiko kwa namna ambavyo watu wengi walifanya machaguo ya wenzi wa maisha na Mungu akakubaliana na machaguo yao.

Ushahidi wa kimaandiko wa namna Mungu aliwachagulia watu wenza wao

Kwa utafiti niliofanya kwenye neno la Mungu mpaka muda wa uandishi wa kitabu hiki, kuna watu watatu tu ambao Mungu aliwachagulia na kuwalazimishia wenzi wao. Na kila mmoja ana mazingira tofauti na mwingine, mazingira yao hayafanani, Mfano:

a) Adamu na Hawa

Mwanzo 2:18-24 (8 Bwana Mungu akasema, Si vema huyo mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye.19 Bwana Mungu akafanyiza kutoka katika ardhi kila mnyama wa msituni, na kila ndege wa angani, akamletea Adamu ili aone atawaitaje; kila kiumbe hai, jina alilokiita Adamu likawa ndilo jina lake.20 Adamu akawapa majina yao kila mnyama wa kufugwa, na ndege wa angani, na kila mnyama wa mwituni; lakini hakuonekana wa kumsaidia Adamu aliyefanana naye.21 Bwana Mungu akamletea Adamu usingizi mzito, naye akalala; kisha akatwaa ubavu wake mmoja, akafunika nyama mahali pake,22 na ule ubavu alioutwaa katika Adamu Bwana Mungu akaufanya mwanamke, akamleta kwa Adamu.23 Adamu akasema, Sasa huyu ni mfupa katika mifupa yangu, na nyama katika nyama yangu, basi

ataitwa mwanamke, kwa maana ametwaliwa katika mwanamume.24 Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja).

Watu wengi sana wakisikia msaidizi wa kumfaa wanadhani ya kuwa mwenza wao akipenda kitu fulani ni lazima na wao wakipende, utakuta mtu akisema “yaani kile anachopenda na mimi napenda”. Siyo sawa! Biblia inasema msaidizi wa kumfaa "opposing mate" ndio tafsiri yake. Mfano mzuri ni wa chupa za maji ya kunywa tulizonazo, chupa na chupa hazifaani, yaani chupa moja haiwezi kusaidia chupa nyingine, lakini msaidizi wa kumfaa chupa ni mfuniko. Kwahiyo msaidizi wako ni kinyume chako “it is the total opposite” ndio maana ya tafsiri ya “msaidizi wa kumfaa”. Chupa na chupa haziwezi kufunikana maji yasimwagike, ila chupa na mfuniko vinafaana, yaani ni mtu na msaidizi wake.

Kwahiyo kimsingi Mungu anapompa mtu mwenzi hata hakuangalia ile ya kusema “anapenda chipsi; napenda chipsi” “anapenda movie na mimi napenda movie” ni kinyume chako. Anakupa kinyume chako ili aweze

kufunika maji yasimwagike, lakini ukiwa na chupa na chupa maji yanamwagika kwa sababu hakuna wa kusaidia mwenzake. Mungu akasema “nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye”, "the opposing mate" Mtu ambaye anapenda vitu tofauti na wewe, mtu ambaye ana malezi tofauti na wewe, mtu ambaye ana makuzi tofauti na wewe ili akukamilishe na ili umkamilishe. Hilo ndilo lengo la ndoa. Haya mambo wanayofundisha huko ya kuwa mnakuwa mnapenda vitu sawa, siyo kweli ya neno la Mungu.

Mwanzo 2:19-20 (Bwana Mungu akafanyiza kutoka katika ardhi kila mnyama wa msituni, na kila ndege wa angani, akamletea Adamu ili aone atawaitaje; kila kiumbe hai, jina alilokiita Adamu likawa ndilo jina lake20 Adamu akawapa majina yao kila mnyama wa kufugwa, na ndege wa angani, na kila mnyama wa mwituni; lakini hakuonekana wa kumsaidia Adamu aliyefanana naye). Mungu alimletea wanyama ili kutokea kwenye hao wanyama huenda akapatikana msaidizi, biblia inasema “lakini hakuonekana msaidizi au wa kufanana naye”. Mungu alimlaza usingizi mzito akatoa ubavu, na Adamu

akatoka kwenye usingizi mzito (Mwanzo 2:22-23). Adamu hakuulizwa na Mungu huyu ni nani, hakusemeshwa na Mungu ya kuwa huyu ni nani. Akaanza kuimba mashairi mwenyewe "Adamu akasema, Sasa huyu ni mfupa katika mifupa yangu, na nyama katika nyama yangu, basi ataitwa mwanamke, kwa maana ametwaliwa katika Mwanamume" (Mwanzo 2:23), Je, aliulizwa kwamba huyu ni nani au ametoka wapi? Alianza kujieleza mwenyewe bila kuulizwa wala kusukumwa.

Moja ya kiashiria kinachoonyesha kuwa huyo jamaa yako yuko kwenye pendo (he is in love) ni pale anapoanza kutiririka mashairi mwenyewe.

Adamu akaletewa msaidizi, mtu wa kwanza kuletewa mwenzi wa maisha ni Adamu. Alileletewa mwenzi kwasababu kulikuwa hakuna mwanamke duniani. Kulikuwa hakuna watu wengine duniani. Kati ya watu ambao huwa nawatamania ni Adamu, Adamu hakutafuta uso wa Bwana amuonyeshe mapenzi yake. Mapenzi ya Bwana yalikuwa pembeni yake, Hawa aliletwa pembeni yake. Kuna wengine hapa bado wamekaa kiadamu Adamu, wanataka Bwana awaletee wenzi pembeni yao.

Adamu aliletewa kwasababu kulikuwa hakuna watu wengine. Kulikuwa hakuna wanawake, kuliwa hakuna watu ambao angechagua kutokea kwao, ndiyo maana Mungu akamletea. Kwa hivyo basi, Kama Mungu atakuletea mwenzi, yaani uamke siku moja umkute pembeni yako, Pole sana, haitatokea! Kama unaomba halafu unasubiri Bwana akuletee pole sana! hiyo haipo, na hauhitaji nabii, maana nabii ndio mimi nimeshasema. Bwana hatakuletea, kwasababu wapo wengi tu.  Kama wa sehemu uliyopo huwaoni, nenda hospitalini wengine wanazaliwa utawaona.Kwahiyo mazingira ya kwanza ili uletewe mwenzi ni lazima kuwe hakuna watu.

b) Nabii Hosea.

Ukisoma kitabu cha Hosea kina sura 14 na kwa faida ya somo hili wekeza muda wa kusoma sura zote. Utakuta Mungu amemfunulia Hosea kuoa mkea aliyemuoa. Na kwa wale ambao wanapenda sana kufunuliwa na Bwana, basi namleta kwako Hosea aliyefunuliwa na Bwana. Bwana akamsemesha katikati ya maombi “Hapo kwanza BWANA aliponena kwa kinywa cha Hosea, BWANA alimwambia Hosea, Enenda ukatwae mke wa uzinzi, na

watoto wa uzinzi;kwa maana nchi hii inafanya uzinzi mwingi kwa kumuacha BWANA”  Bwana akamsemesha Hosea, najaribu kukisia, Hosea inawezekana alikemea, Hosea inawezekana alikataa kama siyo sauti ya Bwana. Bwana akaongea tena! Hosea akaenda kuchukua mke ambaye ni kahaba.

Kwa nini Bwana alimletea Hosea? Mungu alitaka kuyatumia maisha ya Hosea kama njia ya kufundishia (Allegory) na alitaka ili Hosea aweze kutoa unabii vizuri, alitaka asikie (he had to feel it) Mungu anajitangaza ya kwamba ni mume, na taifa la Israeli analiita ni mke wake na amelinunua kwa bei kubwa sana, na kila mara taifa la Israeli lilikuwa linageukia kuabudu miungu mingine. Hicho kitendo cha kumuacha Mungu na kugeukia miungu mingine, Mungu anaita ni ukahaba. Sasa ili uweze kutoa unabii hadi unalia, lazima uwe umepitia haya maisha. Mungu alitaka Hosea atoe unabii vizuri ilibidi amtumie yeye na maisha yake kama sehemu ya kufundisha taifa la Israeli ili waelewe vizuri. Mungu ilibidi amlazimishie Hosea, amuonyeshe mke halafu amlazimishie. Hata kama

hamtaki ilimlazimu, lasivyo asingemuoa huyo mke unabii usingekolea.

Swali: Je, wewe ni nabii ambaye Mungu anataka ayatumie maisha yako kufundishia wengine?

Bwana halazimishi, mpaka ambapo Bwana labda anataka kuyatumia maisha yako kufundisha taifa la Tanzania. Na kama ni hivyo, usitwambie una uchaguzi fulani, ni Bwana atakulazimisha, je uko tayari? Wale ambao wanataka kuisikia sauti ya Bwana mko tayari kuisikia?

c. Yusufu na bikira Mariamu

Mathayo 1 na sura ya 2, Tunajua namna ambavyo Roho Mtakatifu kupitia malaika Gabrieli alienda kuvamia (envade) mahusiano ya watu halafu akapachika na mimba. Biblia inasema Yusufu pia alikuwa mtu wa haki hakutaka kumuaibisha aliazimu kumuacha kwa siri. Kuna jambo la kujifunza hapa; Mahusiano yakivunjika usimuaibishe huyo mtu, usimseme vibaya wala usimdhalilishe. Hasa watu waliookoka maana bado ni ndugu yako katika Kristo, usianze kuzungumza maneno ya ajabu na kumrushia huyo mtu. Mtu wa haki haachi mtu

kwa kumuaibisha. Kama mambo hayajaenda sawasawa bado mwenye haki anabakia kuwa mwenye haki.

Yusufu alikusudia kumuacha kwa siri kwa sababu yalikuwa ni matatizo mazito; kwanza mmepata mimba kabla ya ndoa, fikiria kikao cha wazee wa kanisa pale kanisani ingekuwaje. Pili anaachwa, unaweza ukaelewa? Mungu akaingilia kati akamtokea ndotoni akamwambia usiache kumchukua Mariam mkeo, Kuna kitu cha kiungu kinazaliwa hapo.

Hayo ndio mazingira matatu pekee kwenye biblia ambapo Mungu aliwakutanisha watu na wenzi na akawalazimisha.

Niambie, wewe ni upo kwenye kundi la Adamu? Wewe upo kundi la Hosea? Wewe upo kundi la Yusufu na Mariam? Kwahiyo wote hatupo hapo, kuna sehemu nyingine tupo.

Roho Mtakatifu anazungumza lakini lazima tupate maarifa ya jinsi ya kueneda. Kabla sijaanza kuelezea kwenye kundi unalotakiwa kuwepo, kwasababu wewe sio Adamu na Hawa, wewe sio Hosea na yule kahaba na wala sio Yusufu na Mariam. Hauko kwenye hayo makundi

wala katika mazingira hayo waliyo kuwa, kuna namna yako nyingine. Sasa kwenye hii namna yetu ndio kuna chanagamoto imekuja.

Nilitaka kwanza nianze kukuelezea haya ili wakati unapofika usifanye jambo la kiroho huku ambapo sio pa kulazimishiwa na Bwana, japokuwa wapendwa tunapenda sana, utakuta anasema "yaani Bwana alinitokezea usiku akaniambia" hapo ni kijana wa kiume ameenda kumsemesha binti. Dada akikataa unasema anaipinga sauti ya Bwana. Hata kama Bwana alikutokea kuna huo uhuru wa kumuachia mtu na yeye akasikiliza. Jambo la kiungu litatimia tu, kama sio la kiungu halitotimia, kwahiyo lazima tujue nini kinaendelea.

Huku ambako sisi tupo, ndio kuna huo mchanganyo, ndio kuna hili swali unajuaje kuwa huyu ni mtu sahihi? Kwa sababu Bwana hatakulazimisha, kimsingi kama Bwana hajawahi kukufunulia uwe unawahi kuja kusafisha kanisa, sio rahisi Bwana aje kukufunulia mchumba utakayemuoa au kuolewa naye? Kwa ajili ya kazi ya Bwana hujawahi kabisa kufuniliwa na unataka ufunuliwe tu mke au mume wa kuolewa au kukuoa. Unaweza ukafanya tafakari fupi,

Je, kati ya watu kuokoka na wewe kuoa au kuolewa kipi kikubwa? Bwana hajawahi hata kukufunilia ushuhudie watu hata unaosoma nao au watu wa mtaani kwako, ila Bwana anakufunulia tu kuhusu kuoa.

Upo uelewa ambao tumekaririshwa ya kwamba kila mwanaume ana mtu wake sahihi na kila mwanamke kuna mwanamume wake ambaye ameandaliwa kwa ajili yake. Wapendwa wangu, hiyo siyo sahihi! Hilo fundisho sio kweli. Na hilo limepelekea watu wengine wameingia kwenye ndoa amekaa hata jumla ya miaka saba (7) anasema nimegundua huyu sio sahihi, kwahiyo kumbe ulikuwa unaishi na mke wa mtu? Nimesikia hata wahubiri wanasema nimegundua mtu uliye naye sio kutoka kwa Bwana. Namna hiyo ya fundisho imezalisha utepetepe kwenye mioyo ya wapendwa. Mahusiano siyo kwa watu tepetepe au wachanga kiakili, mahusiano ni kwa ajili ya wanawake na wanaume (Marriage and courtiship is not for boys and girls, its for men and women). Ni kwa ajili ya watu waliokomaa mioyo. Mahusiano yanahitaji kazi, unatakiwa kuyafanyia kazi na ili uyafanyie kazi hupaswi kabisa kuwa tepetepe.

Lazima ujue namna ya kutatua migogoro (Conflict resolution), siyo tu kulalamika “eti hajapokea simu, yupo online na hajanijibu” Acha mambo ya kitoto hayo. Lazima uwe mkomavu wa akili, sasa watu wengi kwa ile “homa ya mtu sahihi”, ikitokea mtikisiko kidogo anasema siyo sahihi, siyo wa Bwana. Kwahiyo inazalisha vijana fulani tepetepe ambao wanataka mtelemko. Nakwambia mahusiano siyo kwa ajili ya watu wavivu.Watu wengi wanafikiri kuna mtu fulani sahihi, ambaye ukimkosa dunia inaisha, ukimkosa umekosea maisha, HAPANA! Hata ukimkosa dunia haitaisha na bado maisha yataendelea.

Fikiria hivi, kama kila mtu duniani ameandaliwa mtu mmoja sahihi, fikiria pamoja na mimi. Tangu dunia imeumbwa hakuna hata mtu mmoja ambaye amewahi kukosea? Sawa, waliookoka huenda watu wote wamepata watu sahihi, je ambao hawajaokoka, hakuna hata mmoja ambaye alishawahi kukosea akaenda kuoa ambaye siyo sahihi? Kwa mfano Mungu amekuumbia dada"W" Halafu ukakosea ukaenda kuoa dada "T" Hakuna mtu tangu dunia imeanza aliwahi kukosea? Watakuwepo wengi. Sasa

kwenye huu mduara wa “Homa ya mtu sahihi” akikosea mtu mmoja anaharibu mlinganyo wote. Kwasababu mimi nikikosea kuoa nakuwa nimeoa mke wa mwingine, maana yake yule wa kwangu sahihi ataolewa na mwingine, na yule aliyemwoa mke wake atakuwa ameolewa na mwingine, na huyu mume wake ataenda kuoa kwingine.

Kwa hiyo mmoja tu akikosea amevuruga mlinganyo wote (equation) wa homa ya mtu sahihi. Nataka kuwauliza tangu dunia iumbwe hakuna aliye wahi kukosea? Wapo wengi tu. Kwa maana hiyo basi, kama kuna mmoja alikosea mwaka 1447 yaani hapa wanaume wanaoa wake za watu, na wanawake wanaolewa na wanaume wa watu.Hiyo siyo sawa! Ndiyo maana nimekuja kuvunja hiyo nadharia maana sio sahihi. Tunachotafuta sio mtu (individual) tunafuata sifa (traits) ndani ya mtu.

MFANO: Mwanajeshi sio mavazi, mwanajeshi ni tabia. Lazima uwe na tabia za kijeshi ndio utaitwa mwanajeshi. Mwanajeshi hata akivua nguo ni mwanajeshi, au akivua nguo anakuwa raia? Hapana! Anabaki kuwa mwanajeshi. Hata ukimuona amevaa jezi ya timu fulani bado ni mwanajeshi. Mwanajeshi ni tabia, ndio maana kabla ya

kupewa mavazi au silaha anafundishwa tabia. Ni hatari sana kuwa na mwanajeshi ambaye unampa bunduki na bado hajawa mwanajeshi atajiua au ataua watu wengine.Hatutafuti mtu bali tunatafuta vitu vilivyopo ndani ya mtu.

Sifa za kuwa mume kwa mfano kila mwanaume anaweza akawa nazo, sehemu nyingine ziko asilimia 90% sehemu nyingine 70% sehemu nyingine 40% Lakini wote tunakua kuelekea kimo cha Kristo, hakuna ambaye ameshafika. Wote tupo kwenye hali ya ukuaji. Hatumtafuti dada fulani, tunatafuta sifa zilizoko ndani ya dada huyo. Kwahiyo usife moyo! Kaa utulie.

Vijana wengi wamekuwa wakiomba sana ili Bwana awafunulie mtu sahihi. Wangapi wanavyoamka asubuhi wanaomba Mungu awafunulie nguo gani wavae? Na wangapi walipovaa walijua ni mapenzi ya Bwana? Hiyo ni kazi ya akili. Biblia katika Mithali 3:5 inasema "Mtumaini BWANA kwa moyo wako wote wala usizitegemee akili zako mwenyewe" Biblia haijasema usizitumie akili zako bali usizitegeme. Sasa kuna vijana walokole kadhaa hawazitegemei na hawazitumii akili zao.

Kuvaa ni tendo la akili, ukivaa Bwana anasema umefanya vyema. Wangapi wakienda mgahawani kuchukua chakula huwa wanaanza kwa kunanena kwa lugha? Huwa ukifika unauliza kuna nini wahudumu wanakwambia kuna hiki na hiki, na unachagua unachotaka. Mungu amekupa akili, tumia! Una akili ya Kristo ndani yako, Yesu anawaza kupitia wewe.

Ukisoma Kutoka 31 utaelewa vizuri, kwa hiyo unapofanya vitu unajiuliza, na kile kitakacho tokezea kitakuwa ni sawasawa kwasababu una akili ya Yesu ndani yako, labda uniambie akili yako ni mbovu sana mpaka uongozwe sala ya toba.

Uelewa wa hiyo homa ya mtu sahihi imepelekea ndoa nyingi kuvunjika na uchumba kuharibika kwa kisingizio hicho. Wapendwa ni mabingwa wa kurohosha (spiritualize). Utakuta mwanaume anasema "amani ya Kristo haipo ndani yangu ya kuendelea kuwa kwenye mahusiano na mwanamke huyu, na inawezekana isiwe amani ya Krsito ni mtu tu kaona mrembo mwingine, ndio amani ya Kristo ikaingilia pale kama kisingizio. Watu hawafanyii kazi mahusiano yao, hawafanyii kazi

uchumba wao, hawafanyiii kazi ndoa zao kwasababu ya homa ya kumpata mtu sahihi.”

Kuna kitabu kwenye biblia ambacho kimejaa muongozo (blue print) wa kimahusiano. Kwa kuwa hatupo kwenye kundi la Adamu na Hawa, wala kwa Hosea na Gomeri wala Yusufu na Mariam basi lazima kuna muongozo wetu mahali. Hicho kitabu kinaitwa Wimbo ulio bora. Kitabu ambacho hakisomwi sana kanisani, kitabu ambacho sio maarufu, na ni kitabu ambacho hakieleweki kwa wengi.

Mtume Paulo akivuviwa na Roho Mtakatifu anamwambia Timotheo katika 2 Timotheo 3:16 “Kila andiko, lenye pumnzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao,na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadabisha katika haki” Kitabu cha Wimbo ulio bora ni kitabu chenye pumzi ya Mungu kwahiyo kinafaa kwa mafundisho, kinafaa kwa kuonya, kuongoza na kuadabisha.

Kwa vile watu wengi sana hawajawahi kukisikia kitabu cha Wimbo ulio bora, wanakiogopa kabisa hata kukifungua. Na wengine hata wakifungua wanatafuta

mstari wa kwenda kutupia kwa mdada au mkaka. Hawajui chochote kuhusu fundisho lililopo ndani yake.

Vitu ambavyo nataka ujue ni kuwa, ndoa ni jambo la kiungu, ni Mungu ndio alianzisha ndoa. Mapenzi mwanzilishi wake ni Mungu. Tabia ya shetani huwa anadakia vitu ambavyo Mungu ameanzisha, halafu anavivuruga anakuwa msemaji mkuu na akiwa msemaji mkuu anapotosha. Na mpaka sasa makanisa mengi yanaogopa kuongelea mada za mapenzi kanisani, Mungu hawezi kuumba kitu asitupatie kitabu cha muongozo. Kwahiyo ukitafuta muongozo wa mahusiano, tangu yanaanza mpaka yanavyoendelea kwasababu hayana mwisho, utayapata kwenye Wimbo ulio bora.

Kitabu cha wimbo ulio bora kina maada kubwa 4 ambazo ni:

Uchumba

Tunatofautiana uchumba unaanza lini, wengine ni urafiki, uchumba mpaka ndoa. Urafiki ni upi na uchumba ni upi. Wengine uchumba ni pale ambapo wanaenda kuvalishana pete, na mara nyingi huwa wanavalishana pete ili wakija

kukuletea kadi za mchango usiwakatalie. Ambapo huo mimi siuiti uchumba. Kwasababu hiyo ni kuhalalisha, mlikuwa kwenye mahusiano tayari, sema tu mnakuja na kupiga magoti madhabahuni ili wakuletee kadi za mchango.

Kuna wengine uchumba ni pale ambapo wamezungumza ya kwamba kuna safari ya maisha tunaenda, nataka kukuoa. Iwe inajulikana au hajulikani kwa mchungaji. Sasa siwezi kusema kipi sahihi au kipi sio sahihi, lakini huwa mnatumia neno mahusiano. Kule yalikoanzia ndiyo panaitwa mahusiano, hapo ndio Wimbo ulio bora. Kwahiyo mada ya kwanza ni uchumba. Huko ndani kuna vipande vinavyoelezea namna ambavyo wamehusiana, mpaka unatoka kwenye kuvutiwa kwenda kwenye kujifungamanisha. Mahali ambapo mahusiano yanaanza kuwa na gundi, wanaanza kuwa imara na kwenda mbele.

Ndoa-

Kuna shughuli ya kufunga ndoa kwenye kitabu cha Wimbo Ulio bora kwa kutumia taratibu na mwenendo wa

kimuktadha. Kuna harusi kabisa ipo kwenye wimbo ulio bora

Fungate - (honeymoon)

Ukienda kusoma Wimbo ulio bora kwa jicho hili utapata kila kitu. Lazima ujue ya kwamba hivi vitu ni baraka. Mungu hawezi tu kuumba kitu halafu akakiacha hewani. Baada ya kufunga ndoa, inaonekana wakiwa kwenye nyakati na maisha ya fungate. Ukisoma kwa umakini kwenye kitabu hiki, utagundua ya kwamba kuna falsafa na kusudio la kiungu nyuma ya wasaa (moment) wa fungate. Ni vyema kuelewa msingi wa kibiblia nyuma ya fungate.

Maisha ya ndoa

Kwenye maisha ya ndoa kuna migogoro. Naomba niwatangazie hakuna mahusiano ambayo hayana migogoro. Kwahiyo ukiingia kwenye mgogoro na kusema huyu sio mtu sahihi, siyo sahihi. Ni vizuri kabisa ujue kuwa mahusiano yote yanapita kwenye mgogoro. Yaani hata kama ungekuwa umeolewa na papa au kiongozi wa heshima kabisa wa ngazi yoyote ya kanisa, bado ndoa

yako ingekuwa na migogoro, hata ukiolewa na Askofu mkuu, nabii au mchungaji au mwalimu bado hayo mahusiano yangekuwa na migogoro. Kwahiyo uwe na ukomavu wa akili kujua hivyo vitu. Migogoro inanogesha pambano ukiwa na maarifa utatumia mgogoro kama njia ya kuimarisha mahusiano. Kuna watu migogoro inawavusha na kuna watu inawaangusha.

Kuna hiki kitabu nimekiandika kinaitwa mahusiano 101, kina maelezo zaidi. Kuna mambo ambayo unayatazama kwa huyo mtu ambaye unataka kuanzisha naye mahusiano. Vitu vifuatavyo ndivyo vya kutazama, kutafuta au kuangalia unapotaka kuanzisha mahusiano.

Mvuto

Wimbo Ulio Bora 1: 1-4 “Wimbo ulio bora, wa Sulemani. Kubusu na anibusu kwa kinywa chake. Maana pambaja zako zapita divai. Manukato yako yanukia vizuri;jina lako ni kama marhamu iliyomiminwa;kwahiyo wanawali hukupenda. Nivute nyuma yako, na tukimbie; Mfalme ameniingiza vyumbani mwake. Tutafurahi na kushangilia; Tutazinena pambaja zako kuliko divai;

ndiyo, ina haki wakupende" Ni hali ya kitamaduni anayoitumia mtu kuelezea kuvutiwa na mtu. Anayezungumza maneno ya mstari hapo juu ni Mwanamke.

Kwa wale wanaofuatilia mambo ya utamaduni wanajua. Watu kutoka Mashariki ya Kati kusalimiana kwa busu kwao siyo kitu cha ajabu. Ndio maana mtume Paulo akawaandikia Wakoritho katika 2Wakorintho 13:12 "Salimianeni kwa busu takatifu". Ila siwezi kuja hapa Tanzania na nikawaambia ya kuwa salimianeni kwa busu takatifu kwasababu sio jambo linaloendana na tamaduni za Kitanzania. Kwahiyo busu aliyoiongelea Paulo usije ukaitengenezea mawazo yako, ni busu ambalo kwenye utamaduni wao ni kitu cha sawasawa. Kwenye tamaduni zingine inaonekana kama kusalimiana kwa kushikana mikono.

Mfano, Paulo angekuwa anawaandikia watanzania angesema salimianeni kwa kushikana mikono mitakatifu. Angekuwa anawasalimia ndugu zangu wa kusini angesema, salimianeni kwa kupiga magoti matakatifu. Lengo ilikuwa ni kuonyesha ya kuwa ni jambo la

heshima. Huyu mwanadada anaposema “kubusu na anibusu kwa kinywa chake” yuko kwenye kufikiria, anaelezea mvuto. Kitu cha kwanza tunachojifunza ni kwamba, hatuchukui tendo lililofanyika, tunachukua somo (funzo). Ukiendelea kusoma utaona mwanamke akielezea sifa ya kuwa “Tazama u mzuri, mpenzi wangu, u mzuri, macho yako ni kama hua” (Wimbo ulio bora 1:15). Kwa sasa huwezi kumkatia mpenzi wako mistari unamwambia “uso kama farasi”, utaachwa mtumishi wa Bwana. Tunachukua funzo. Kwa hiyo anachokisisitiza huyu binti ni kuwa amevutiwa. Mkazo uko kwenye mvuto na siyo busu hasa hasa!

Kwenye utamaduni wao kuvutiwa ni mpaka mtu akubusu ndiyo maana anatamani busu lake. Ni kama hapa kwetu unatamani mkaka fulani akija kukusalimia akushike mkono. Lazima ujue hiyo busu imetokea kwenye mazingira gani. Jambo la kwanza ambalo linatufunukia kwa haraka kitu cha kwanza ni mvuto. Hili jambo ni la kiroho kabisa, mwingine atajiuliza kwanini “Pastor” hajaongelea la maombi. Mwingine anavutiwa na sauti yake anavyoimba, ni sawa kabisa lakini sauti pekee

haitoshi, labda kama mnataka kufungua bendi, hapo ni sawa. Mungu hawezi kukulazimisha kuingia kwenye mahusiano, kuolewa au kuoa mtu ambaye hujavutiwa naye, Mungu hawezi kufanya hivyo.

Mfano: Adamu alijielezea kuvutiwa na Hawa, ukiona kwenye Mwanzo 2:23-24 aliongea mashairi fulani ambayo sijawahi yaona duniani. Alitamka masahairi fulani mazito sana, “ Adamu akasema sasa huyu ni mfupa katika mifupa yangu, ni nyama katika nyama zangu ataitwa mwanamke”. Adamu alikuwa amelala lakini alivyoamka na kuona mtu mzuri mbele yake alivutiwa naye sana.

Mfano: Mwanzo 29:17-20 (Naye lea macho yake yalikuwa dhaifu, lakini Raheli alikuwa mzuri wa umbo, na mzuri wa uso) Mbele ya Yakobo kulikuwa na warembo wawili Raheli na Lea lakini Yakobo akampenda Raheli kwasababu ya umbo na uso na alikuwa tayari kufanya lolote ili aweze kumpata. Miaka saba ilikuwa si kitu kwake, ni kama kusoma elimu ya msingi kwa miaka saba (7).

Ni vizuri kujua aliyeumba hayo maumbo ni Bwana, Zaburi 139:13-14 (Maana wewe ndiwe uliyeniumba mtima wangu, uliniunga tumboni mwa mama yangu. Nitakushukuru kwa kuwa nimeumbwa kwa jinsi ya ajabu na kutisha) Lazima mtu ambaye unaingia naye kwenye mahusiano ya kuelekea kwenye ndoa uwe umevutiwa naye, lazima kuwe kuna uajabu na hali ya kushangaza.

Anayetoa taarifa hapa, inawezekana ameripoti kutokea kwenye jicho la muonaji, kwasababu pia kuna watu ambao wanapenda macho fulani hivi, ambayo inawezekana Yakobo hayapendi. Ila kuna jamaa mwingine angevutiwa na hayo macho, kwahiyo macho ni dhaifu kwa Yakobo lakini yanaweza kuwa ni nguvu kwa mwengine. Tumeumbwa kwa namna ya ajabu ya kushangaza ili tusigombanie mtu; ili kila mtu awe na watu anaowavutia kwa upekee wake na upekee wao na/au mtu aweze kuwavutia wengine kwa upekee wake. Kuna watu wanapenda watu warefu, kuna wengine wanapenda watu wafupi. Kuna watu wanapenda wanene, wengine wanapenda wembamba, kuna wengine wanapenda weusi,

wengine wanapenda weupe. Kuna wanaopenda wanaofuga ndevu na kuna wasiopenda ndevu.

Kuvutiwa sio tamaa ya mwili, sizungumzii kuwaka tamaa ya mwili hivi ni vitu viwili tofauti. Kuvutiwa ni ile ambayo Timotheo anaandikiwa “Ni neno la kuaminiwa;mtu akitaka kazi ya uaskofu, atamani kazi njema” 1Timotheo 3:1. Neno “kutamani” haimaanishi tamaa mbaya inamaanisha tamanio takatifu (holy desire). Ushawahi kumpenda mtu ukamfurahia, sio kwamba unataka ufanye naye mapenzi ila unamfurahia unampenda na hautaki baya lolote limpate. Ukiulizwa unaweza usijue kwanini unavutiwa na yule mtu. Sio kwamba unataka uende kulala naye hapana! Lakini umevutiwa naye tu.

Hata hivyo mvuto sio hitimisho la kuanzisha mahusiano. Mithali 6:25 “Usiutamani uzuri wake moyoni mwako; wala usikubali akunase kwa kope za macho yake” Mithali 31:30 “Upendeleo hudanganya, na uzuri ni ubatili. Bali mwanamke amchaye BWANA, ndiye atakayeheshimiwa”. Kuna wengine wananaswa kwa kope. Kope zinakukamata nafsi yako. Huwezi tena kutafiti kujua mambo yote ya msingi unaishia kwenye

kope tu unampenda na kumuoa. Usifanye hitimisho kwa kutazama mvuto maana hudanganya, sisemi usivutiwe! Mvuto ni kama bendera inayokuita ili uweze kuchunguza ujue ndani kuna nini.Usiende na kuweka kambi bila kujua ndani ya huo mvuto kuna nini, ndio umevutiwa ila kuna vingine vya kuzingatia.

Usafi

Wimbo Ulio bora 1:3 “Manukato yako yanukia vizuri; jina lako ni kama marhamu iliyomiminwa; kwahiyo wanawali hukupenda” Maana yake ni kwamba alikuwa msafi. Paulo anamwambia 1Timotheo4:12 “Mtu awaye yote asiudharau ujana wako, bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi na mwenendo,na katika upendo na Imani na usafi” Lazima kuwe na hali ya usafi. Usiishie kuvutiwa tu. Hasa kwa watoto wa kiume, wengine wanavaa nguo ya ndani “boxer” moja kwa wiki nzima, lazima uwe mtulivu asikutishe na swaga au miondoko ya ujana.Wengine hawajui hata kupangilia vyumba vyao wanaacha chumba hakitamaniki yaani ni mchanganyiko kila sehemu. Kama mtu hawezi kupanga chumba chake uwezekano mkubwa ni kwamba hawezi kuyapanga

maisha yako pia. Asikutishe na anavyotembea au anavyotunisha misuli, maisha hayaongozwi na misuli ya kifua, yanaongozwa na misuli ya kichwa. Wakati wewe upo “gym” unatunisha misuli na wengine wapo “gym” ya kiroho. Maisha hayaangalii unatunisha misuli kiasi gani ili yasogee, unaweza ukawa umetunisha misuli na hauna maarifa ukapigika, kwahiyo usitishwe na uzuri. Na sisemi kwenda “gym” ni vibaya, hapana! Mazoezi ni mazuri sana kwa ajili ya afya, usiishie kwenda gym pekeyake haitoshi.

Kijana usiangalie binti anayetembea kwa maringo na kutingishatingisha wala usitishike naye, anaweza akawa wa kawaida sana. Asikutishe na sauti yake ya kumtoa nyoka pangoni, dada mmoja akiongea hivi mpaka unasikia tetemeko la ardhi, isikutishe baba. Uzuri hudanganya, inawezekana kuna uongo nyuma ya huo uzuri, inawezekana kuna uongo kwenye hizo lipstick na huo wanja, Usidanganyike! Vijana wengi sana wamekamatwa hapo usidanganyike na “selfies”, kuna maisha baada ya kupiga picha. Uzuri hudanganya, kope zinadanganya, piga hatua kubwa zaidi ya kupima usafi, je ni msafi?

“Kwahiyo wanawali hukupenda” Wimbo ulio bora 1:3

Wanawali wengine walikuwa wamevutiwa naye. Ni kama huyu dada anayezungumza kwenye kitabu cha Wimbo Ulio bora anasema nina ushindani na wasichana wengine. Mimi nakupenda lakini kuna wadada wengine wanakupenda, kwasababu jina lako ni kama marhamu iliyomiminwa. Kwa lugha ya biblia ilikuwa ni kumimina marhamu, kwa lugha ya sasa hivi ni sawasawa na kupuliza (spray). Anasema “jina lako ni kama…” kwahiyo anataka tuelewe kwamba “perfume” ikibonyezwa tutaelewa jina lake lina harufu gani. Tukielewa perfume iliyomiminwa ndio tutaelewa uwezo wa jina la huyu jamaa. Anasema jina lako linatoa harufu, jina lako linanuswa, jina lako likitajwa mabinti wote wanafurahia. Kuna mwanasiasa na kiongozi ambaye hapo kale alikuwa ni mwimbaji, aliwahi kusema kuhusu majina kwenye moja ya nyimbo zake, “Jina langu linavuma kwenye mitaa, jina langu lina hadhi ya kisupa star”. Majina yanavuma, majina yanasikika, majina yanatoa harufu.

Ukisoma Mithali 22:1 “Heri kuchagua jina jema kuliko mali nyingi; Na neema kuliko fedha na dhahabu” Kumbe

unaweza ukachagua jina. Kuna majina mengine huwezi chagua. Mimi nilivyozaliwa nikakuta naitwa “James” sikuchagua lakini baadae ukikua unaweza ukabadilisha. Kuna namna haya majina tunayapata. Wazazi wanatoa majina kwasababu ya tamaduni kama kimapokeo. Namna ya kimazingira mfano, nilimzaa katika uchungu. Wapo kina Shida, Masumbuko,Tabu, Masanja, Mabula na wengineo, ni kwasababu ya mazingira fulani, na hayo mazingira yanaweza yakawa mazuri au mabaya. Kutoa majina kinabii (prophetic naming) mnapata mtoto na mnamwamini Bwana ya kwamba tunatamani kitu fulani kitokee kwake, kwahiyo mnampa hilo jina, akikua anaambiwa sababu ya yeye kuitwa hivyo ili awe hivyo... Mfano jina Yesu, lilikuwa ni jina la kinabii.

Sasa hapa sizungumzii majina unayozaliwa nayo, bali ninazungumzia majina ambayo huwa yanawekwa kuelezea jina. Kwa mfano nikitaja Rahabu, nini kimekuja kwenye kichwa chako (kahaba) sasa hili ndilo jina ninalolizungumzia. Hadi leo Rahabu amekufa lakini bado tunasikia harufu ya jina lake. Lazaro akitajwa kinachokuja akilini ni Umaskini. Ukisikia Daudi kuna harufu inakuja.

Sasa nataka utambue ya kuwa jina lako likitajwa kuna harufu inasikika, lazima kuna maelezo yanapatikana. Kama jina Rahabu likitajwa harufu inayosikika ni kahaba, bado katika Agano Jipya katika Waebrania 11:31 “kwa Imani Rahabu, yule kahaba” inaendelea kusisitiza harufu ya jina lake. Harufu inabakia japokuwa amejitokeza kwenye orodha ya mashujaa wa imani.

Kwa hiyo ukivutiwa naye hakikisha unamnusa jina lake kama ni msafi. Kimsingi sizungumzii jina nazungumzia tabia. Umevutiwa ndiyo, lakini ana harufu gani? Kama umevutiwa na mguu basi uwe ni mguu unaopeleka habari njema, sio miguu inayotembea tembea kwenye ukahaba. Ninachosema ni kwamba, majina yanatoa harufu, nenda kamnuse huyo mtu. Kifedha ananukiaje, kimaombi ananukaje? Na kama unataka kujua harufu vizuri nenda kwenye mkusanyiko wa watu na uulize jinsi wanavyomzungumzia mtu fulani, lazima utasikia harufu ya jina lake.

Na ninawaambia wadada, wakaka huwa wana vikao na huwa wananusa sana majina ya wadada kwenye vikao vyao. Wakaka niwaambie pia, wadada huwa wanaongea

na kuwajadili, sasa sijajua harufu za majina yenu huwa zinakuwaje kwenye hivyo vikao. Badala tu ya kunusa harufu za wengine hakikisha unatengeneza harufu yako (Build your character). Kuna watu ambao watasema jina lako linatoa harufu safi, jina lako lina hadhi ya ki-super star. Ndio maana wanawali wanakupenda. Kuna majina yana harufu nzuri sana, ila kuna jina likitajwa harufu yake sio nzuri kabisa.

Wengine inawezekana hili somo hamtalitumia mwaka huu au mwakani, mtalitumia miaka mitano ijayo, Bwana asifiwe kwa sababu mna muda wa kutengeneza harufu zenu. Hata kama utatumia miaka kumi ijayo, una muda wa kutengeneza harufu ya jina lako. Niko hapa kukwambia, tengeneza jina lako, tengeneza harufu ya jina lako.

# SURA YA TATU: NAMNA YA KUANZISHA MAHUSIANO.

Katika kipengele hiki tutaangalia nini cha kuangalia au kuacha na nini cha kujiandaa. Baada ya kupasua ile nadharia ya kutafuta mtu sahihi, ya kwamba hakuna mtu ambaye ameumbwa kwa ajili yako na wewe umeumbwa kwa ajili yake, huo sio ukweli. Ukiwa na uelewa wa namna hiyo, badala ya kutafuta mtu sahihi, wewe ndio unatakiwa kuwa mtu sahihi, ambapo mtu sahihi unayemtafuta na yeye anatafuta mtu sahihi. (Be the right person that the right person is looking for). Kuna mtu sahihi ambaye kila mara unamtafuta lakini acha kumtafuta huyo mtu sahihi wewe ndiyo uwe mtu sahihi ambaye mtu sahihi unayemtafuta anamtafuta. Wewe ukishakuwa mtu sahihi basi mtapatana tu.

## Namna ya kuwa mtu sahihi

i) Kujitambua kibinafsi

Lazima ujitambue wewe ni nani. Wimbo ulio bora 1: 5-6 “Mimi ni mweusi-mweusi, lakini ninao uzuri, Enyi binti za Yerusalemu, Mfano wa hema za Kedari, Kama mapaziayakeSulemani. Msinichunguze kwa kuwa ni mweusi-mweusi, Kwa sababu jua limeniunguza. Wana wa mamangu walinikasirikia, Waliniweka niwe mlinzi wa mashamba ya mizabibu; Bali shamba langu mwenyewe sikulilinda” Anajitambulisha anasema "mimi ni mweusimweusi lakini ninao uzuri" tafsri yake ni kwamba, ninajua mimi ni nani, na ninajua mimi si nani, ninajua nina uzuri lakini vilevile ninajua mimi sio mweupe.

Namna ya kujiandaa vizuri ili uingie kwenye mahusiano ni lazima ujue wewe ni nani na ujue wewe sio nani. Kwenye vipimo vya uzuri vya wakati huo kwa mujibu wa hili andiko "mimi ni mweusi-mweusi" ni kama anawaambia wale wengine ya kuwa, tukijilinganisha mimi na nyie, ni kama vile wanataka kunidharau kwa ajili ya weusiweusi wangu, ni kama tukisimamishwa tushindanishwe mbele ya huyu kijana, ni kama vile

wanataka kumwambia usioe huyu kwa sababu ni mweusimweusi. Lakini huyu binti ana ujasiri sana, anamwambia huyu kijana ukinikosa mimi utakuwa umekosa kitu cha thamani sana.

Ninatamani sana mabinti wa namna hii, wenye ujasiri mkubwa. Anaweza kukutazama machoni na kukuambia kwa ujasiri ya kwamba usiponioa mimi umepungukiwa sana. Hivi ndivyo unatakiwa uwe kwasababu unajua wewe ni nani, siyo unatembea ukisikia tu kijana amepiga mluzi unasema "eeeh! Mimi", hujiamini! Huyu dada anajua kabisa ya kuwa alikuwa hafikii viwango vya uzuri vya wakati ule. Kuna viwango fulani vya uzuri ambavyo vinakuwa vikionekana kwenye Tv na mitandao ya kijamii. Ukijiangalia na kujipima kwa kutumia viwango hivyo unasema wewe haufai.

Lazima pia ujue wewe sio nani. Mimi ninajua ni mchungaji, mtumishi wa Mungu. Kwahiyo ninajua mimi ni nani na mimi sio nani. Lazima ujue wewe ni nani na wewe sio nani, lazima ujue kuchora huo mstari.

Kwa vipimo vya uzuri wa wakati huo, inawezekana uzuri ulikuwa unapimwa kwa rangi, anasema mimi ni mweusimweusi maana yake mimi sio mzuri kwa vipimo vya wakati huo. Ni kama anamuambia yule kijana ya kwamba ukiwafuata hao wengine kuna kitu utakuwa umekosa.

Lazima mdada uwe na ujasiri huo, siyo ukiongea unasugua sugua miguu chini kama ishara ya hofu au kutojiamini, lazima ifike mahali useme mimi ni mweusimweusi lakini ninao uzuri, mimi ni zaidi ya rangi ya ngozi. Lazima ujue umebeba nini. Wewe ni zaidi ya nywele za bandia, wewe ni zaidi ya lipstick, wewe ni zaidi ya rasta, wewe ni zaidi ya viatu. Wewe thamani yako haiko kwenye vitu. Watu wanaojitambua wanavipa vitu thamani, watu wasiojitambua wanapewa thamani na vitu.

Kuna mtu ili aonekane ni wa maana inabidi apige picha na awe na aina fulani ya bidhaa (kama vile aina ya simu) kwa pembeni, aonekane na aina hiyo ya simu ndiyo tumuone wa thamani. Kuna watu anaenda kupiga picha pembeni ya gari ili tumuone wa thamani. Kuna watu lazima avae aina fulani ya jeans ili tuone thamani yake,

yaani yeye thamani yake anapewa na lebo ya jeans; Ukweli ni kwamba wewe ni zaidi lebo za mavazi.

Kuna wadada wanasema lazima avae aina fulani za nywele ndio aonekane wa thamani. Wewe ni zaidi ya nywele, wewe ni zaidi ya saa. Wewe siyo vitu vya nje, wewe ni wa thamani, wewe ndio unavipa vitu thamani sio vitu vinakupa wewe thamani, lazima ufike hapo ujitambue wewe ni wa muhimu kiasi gani. Ukifika hapo unaweza ukasema mimi ni mweusimweusi lakini ninao uzuri.

Ni kweli sina viatu vya hivi lakini ninao uzuri; Ndiyo sina ile nywele ya bandia ya bei lakini ninao uzuri; ndiyo sijaweka lipstick lakini ninao uzuri; ndiyo sina aina fulani ya suti lakini ninao uzuri kwa sababu wewe ni zaidi ya mavazi. Mtu ambaye ameshaingia kwenye mahusiano au nini cha kujiandaa kuingia jijue wewe ni nani. Wewe sio mtu wa kwenda na fasheni, wewe ni zaidi ya vitu!

## Wewe ni nani

Mwanadamu ni roho yenye nafsi na inaishi ndani ya mwili. Kwanza, wewe ni roho, halafu pili, wewe ni nafsi, mwili ni kasha ambapo wewe ndimo unakaa. Kwahiyo

lazima ile roho ijitambue, na roho ijitambue ni jambo moja tu ambalo linahitajika ambalo ni kuokoka. Yaani mtu ambaye hajaokoka ni mtu aliyechoka; Mtu ambaye hajaokoka anaweza akawa mnyama dakika yoyote ile. Yaani mwanamke yoyote ambaye hajaokoka anaweza kuwa mnyama dakika yoyote ile. Mwanaume ambaye hajaokoka anaweza kuwa mnyama dakika yoyote ile. Kinachobadilisha ni mtu anapokuwa ametia nanga kwenye maisha ya umilele, mtu anapokuwa na uhakika wa maisha ya umilele yanaamua aishije sasa hivi.

Kwahiyo wewe sio mwili, wewe ni roho. Maandalizi ya kwanza ya kuingia kwenye mahusiano ni kuokoka. Kama una kamchumba kanajulikana au hakajulikani ila hakajaokoka pole, umeenda chaka. Kukaa na mtu ambaye hajui umilele wake, atajua kesho? Kama tu milele hajui atakuwa wapi, atajua kesho atakuwa wapi? Usipoteze muda wako. Unamwambia "I love you" ila anaenda motoni. Kuna faida gani kufunga safari ya maisha yote na mtu ambaye hayapendi maisha yake?

Biblia inasema mwanaume ni kichwa cha mke wake, kwanini uongozwe na mtu ambaye anaenda motoni.

Kwanini uzae watoto na mtu anayeenda motoni, unajisikiaje? Hiyo tu inaonyesha wewe mwenyewe ni wa hali ya chini sana. Lazima mtu awe ameokoka. Wokovu ni jambo la kujivunia, sio kitu cha kishamba. Kuwa na uhakika na Mungu wako.

Nipozungumza hivyo ninamaanisha lazima ujue wewe ni wewe ni roho. Kama kuna mtu aliwahi kukutokea (kukutongoza) na hajaokoka, nenda kampige injili. Kama upo kwenye mahusiano na mtu ambaye hajaokoka nenda kampige chini. Wengine wanasema akishanioa ataokoka, usijidanganye. Mara nyingi mazungumzo mabaya huharibu tabia.

## Wapi pa kutafuta

Kuna uelewa fulani kwenye mawazo ya watu ya kwamba lipo soko la ndoa, katika ulimwengu wa mwili na dunia isiyoshikika. Kuna hali fulani ya uelewa imekaa mioyoni mwa watu. Ukiwa na uelewa huo kwamba kuna soko la ndoa na ukaenda sokoni kama mnunuaji, utakutana na bidhaa imewekewa "package", saa nyingine wameifungwa kitapeli.

Soko la ndoa linaua, kwasababu unakutana na watu ambao ni matapeli, uelewa wa soko la ndoa umedanganya wengi. Watu wanaanza kuji-package, mtu akigundua wakati wake umefika ndiyo anaanza kuji-package, anaanza kuabudu kwasababu kunakuwa na aina fulani ya mtu anawinda ili apate bidhaa hiyo. Usiingie kwenye mahusiano kwa sababu ya karama. Mnazijua karama za Roho Mtakatifu? Ndoa haiendeshwi kwa karama, karama ni kwa ajili ya kujenga mwili wa Kristo, labda kama unatafuta mchungaji msaidizi na si mke wala mume. Ndoa inaendeshwa kwa tunda la Roho. Kama hulijui kalitafute mwenyewe kutoka katika kitabu cha Wagalatia 5.

Maisha yanaendeshwa na tunda la roho sio karama. Wengi wanaji "package" kwenye karama kwa sababu tunda ni tabia. Sokoni hawaendi kwa kunena kwa lugha, ndani hamuishi kwa kunena kwa lugha. Suala la soko la ndoa ni uongo ambao unasababisha watu wawe wasanii na wandanganyifu. Kuna mtu anajua muda wangu wa kuingia sokoni unafika kwahiyo anaanza

kujipambapamba, unawinda na yeye anawinda, unakuta wote wameoana wasanii tu. Acheni maigizo!

## Sehemu ya kupata mwenzi

Wimbo ulio bora1:6 “Msinichunguze kwa kuwa ni mweusi mweusi, kwasababu jua limeniunguza.Wanan wa mamangu walinikasirikia,waliniweka niwe mlinzi wa mashamba ya mizabibu;bali shamba langu mwenyewe sikulilinda” Huyu mwanaume amempata binti kwa kumuona shambani, Kama unatafuta mahali pa kuoa nenda shambani. Angalia Wimbo Ulio bora 1:7-8 “Nijulishe, ee mpendwa wa nafsi yangu.Ni wapi utakapolisha kundi lako. Ni wapi utakapolilaza adhuhuri. Kwanini niwe kama aliyefungiwa kidoto,karibu na makundi ya wenzako. Usipojua wewe uliye mzuri katika wanawake, shika njia uzifuate nyayo za kondoo.Na kuwalisha wana mbuzi wako karibu na hema za wachungaji” Mwanaume na yeye anapatikana shambani na mwanamke yuko kwenye shamba la mzabibu.

Sehemu ya kupata, kuona, kufunuliwa, kuvuviwa, kuonyeshwa, kukuguswa au kupata amani ya moyo, kuwiwa ni shambani. Sasa kwenye mazingira yao

walikuwa kwenye mashamba ya mizabibu na kuchunga kondoo lakini pointi ni kwamba sio lazima uwe kwenye shamba la mzabibu au kuchunga mbuzi na kondoo, lakini ni kwenye shughuli za uzalishaji; kwenye kuzalisha matokeo huko ndipo utapata mwezi.

Huko hakuna wasanii, maana huwezi kuigiza kazi wala kuigiza kuzalisha matokeo. Watu wasio na tabia ya kufanya kazi hawatafanya kazi, hawatayafanyia kazi mahusiano. Mahusiano ni kazi: kujitoa, kuomba, kujifunza. Watu wasio na tabia ya kufanya kazi hawawezi kuyafanyia kazi mahusiano na kwasababu hiyo ukiingia kwenye mahusiano na mtu ambaye ametoka kwenye soko la ndoa hayo mahusiano yatavunjika kwasababu hawana msuli wa kufanya kazi. Uvivu kazini ni uvivu kwenye mahusiano. Mtu asiyefanya kazi yeye mwenyewe ndiyo kazi ya kufanya, yaani ukimuoa mtu asiyefanya kazi utakuwa umepata kazi. Yaani wewe mfanya kazi umeingia kwenye mahusiano na mtu asiyetaka kufanya kazi unakuwa na kazi mbili, kazi yako na yeye mwenyewe pia ni kazi. Pointi yangu ni nini? Shambani ni mahali popote pa uzalishaji na kuleta matokeo. Muangalie

kanisani, kuna watu huwa ni mabishoo kanisani wanashindwa kuwa na uhuru mbele za Mungu.

Mwanamume ambaye hawezi kumwabudu Mungu, mwanaume ambaye hawezi kujiachia kwenye mamlaka kuu, hawezi kujiachia kwako. Angalia bidii yake anapokuwa kwenye nyumba ya Mungu. Huu weusi ulio nao sio asili yangu ni matokeo ya kazi. Tafuta binti ambaye hadi nywele zimeenda upande kwa sababu ya kazi chukua “hicho kifaa”. Angalia wakaka ambao wako “busy” kwenye nyumba ya Bwana, kuna vitu wanafanya achana na wale waliokaa wameshikiliwa kwenye simu zao na wanawasiliana tu muda wote (chatting).

# SURA YA NNE: UMRI WA KUINGIA KWENYE MAHUSIANO

Jambo la msingi sio umri kwa maana ya namba, bali ni ukomavu (maturity). Kinacho tafutwa sio umri, bali ni ukuaji. Kwahiyo kuna watu ambao wameweka umri ya kwamba ukiwa na umri fulani unaweza kuingia kwenye mahusiano. Kimsingi wanachokitafuta sio ile namba, wanachokitafuta ni ukomavu au ukuaji unaombatana na hiyo namba. Wanahisi kwamba wanatajaria ukiwa na umri fulani uwe na ukomavu fulani. Tunakutarajia ukiwa na miaka 25 kuna aina fulani ya mawazo yawe yameingia ndani yako. Tunakutarajia ukiwa na miaka 25 kuna aina fulani ya kufikiri iwe imeingia ndani yako.

Kuna watu wengine wanapata ukomavu wa akili hata kabla ya umri. Inawezekana ni sababu ya malezi, mapito, bidii na kujifunza. Unagundua kabisa huyu mtu ni mkomavu kuliko huyu hapa. Suala sio kufikisha umri fulani, kuna watu ambao wamefikisha umri lakini kuna aina fulani ya ukomavu wa akili bado hawajaipata. Yaani kuna watu wana miaka 40 lakini bado ni wavulana, ni

wavulana wa miaka 40 na kuna watu ni wanaume wa miaka 18.

Kwahiyo anayepaswa kuingia kwenye mahusiano ni mtu mwenye ukomavu wa akili. Mahusiano ni kwa ajili ya watu wawili, ndoa ni kwa ajili ya watu waliokomaa. Kuna vitu vitakuibukia huko ndani na utalia wenyewe, unakuta mwanaume mzima lakini analia.

Mtoto wetu wa kwanza anaitwa Joshua-Vision alipata changamoto ya afya, akapofuka. Alivyopofuka akapata mtindiko wa ubongo, halafu sehemu ya mguu wake wa kushoto ukalemaa. Ni mtoto aliyekuwa anaona na alikuwa ameshaanza kusoma shule. Sasa haoni, hawezi tena kuongea. Na jambo hilo limetokea sio usiku mmoja, amekaa ICU wiki nzima. Umepewa taarifa mtoto wako ni kipofu, na yote hayo yametokea mke wangu akiwa ni mjamzito.

Kama mwanaume unafanyaje? Unaanza kulia? Baada ya hapo mama amejifungua unatakiwa kuja kumuelezea kwamba mtoto wake anaumwa, halafu unamsaidiaje asimame vizuri. Sio unaulizwa unasema mimi sijui sasa.

Sasa aulizwe nani? Baada ya kutoa taarifa kwake kwamaba mtoto ni kipofu na hawezi kutembea, tunafanyaje? Hospitalini walisema kwamba ni ugonjwa ambao hautibiki. Wakatushauri tutafute wanasaikolojia watueleze namna ya kuishi na huyo mtoto. Inahitaji mtu mwenye ukomavu wa akili kukabiliana na suala la namna hiyo. Na ndugu zako nao wanakuja, ndugu wa kila rangi, wengine hawajaokoka na wengine wameokoka. Wengine wanakwambia uende kwa mganga, wengine wanasema tumelogwa. Kila aina ya mtu anakuja! Na hiyo safari mnatembea sio wiki 2, sio miezi 3 ni mwaka mzima mtoto yupo namna hiyo.

Mwanzoni unaweza ukakataa ila baadae unaweza kukata tamaa. Lazima uwe umekomaa, uwe unaweza ukasimamia misimamo yako. Mpaka sasa huyu mtoto anatembea, anaona na yupo shule sasahivi. Pointi yangu ni kwamba, ukipita kwenye nyakati za namna hiyo unafanya nini, unaanza kulia? Hapana, unatakiwa uwe na akili za kukabiliana na hali hiyo.

Kwenye ndoa yenu anaweza akatokea mjomba wako akasema mimi simpendi huyu binti, miguu yake ni kama

inarudi nyuma. Unakabiliana nalo vipi jambo kama hilo? Au wanakuja jopo la dada zako, wanakwambia kaka tunaona huyu wifi pua yake inaelekea kulia, unaweza ukacheka ukaona ni kitu rahisi, hapana sio kitu rahisi. Au mama yako mzazi anakwambia mwanangu huyu mke nimeonyeshwa na Bwana kuwa sio wako, unatakiwa uwe na akili zilizokomaa kukabiliana na suala hilo. Sasa ukiwa na akili zako za kitoto watakuja watu waingilie ndoa yako ndio maana ndoa ni kwa ajili ya wakomavu. Mtu ambaye anaweza akasema hapana kwa mtu yeyote hata kwa wazazi.

Dada zangu, usiende kuolewa na mvulana, usiingie kwenye mahusiano na mvualana. Wavulana ni wale ambao ukiongea kitu tu wanasema, ngoja niongee na shangazi, ukiwa na kivulana cha namna hiyo achana naye. Mwanaume anasimamia maamuzi yake, hasubiri kufanyiwa uamuzi na ndugu au wazazi wake. Lazima awe ni mtu anayejitambua kibinafsi, awe mtu wa kazi, aweze kufanya maamuzi na kuyasimamia.

Wimbo Ulio bora 1:3 Huyu mwanaume sio kwamba alikuwa amefungwa kamba, kwa mujibu wa maelezo ya

huyu binti, jamaa alikuwa anapendwa na mabinti wengi, alikuwa anapendwa na warembo wengi pale mtaani. Lakini huyu mwanaume kutokea kwenye wanawake wengi waliopo akamchagua huyo binti na akasimamia maamuzi yake.

Sio unakuwa na mvulana kwenye mahusiano akiona kitu kidogo tu anasema hasikii amani ya Kristo. Sio hata amani ya Kristo ni upumbavu umemjaa moyoni, ameona mwingine na akashindwa kusimamia maaumuzi yake. Ndoa huwa ni maamuzi.

Upendo ni maamuzi, kuna kiwango cha upendo ambacho ni hisia. Upendo ambao unatunza ndoa ni maamuzi. Sio ambao ukiomuona mtu unasema moyo unakudunda, unachanganyikiwa. Wasichana wanasema nikimuona mpaka nasisimka. Ndoa haitunzwi na upendo wa kumuona mtu mpaka unasisimka. Upendo ni maamuzi. Upendo sio hisia, hisia zinakuja na kuondoka. Hisia hazidumu, ndio maana haukasiriki muda wote. Kama upendo wako umejengwa kwenye hisia maana yake huwa unakuja na kuondoka, na hauwezi kujenga mahusiano kwenye ngazi ya hisia, lazima ufike ngazi ya maamuzi.

Ukiniuliza kwamba unampenda mama mchungaji nikikujibu kulingana na hisia naweza nikakwambia ya kuwa sijui, lakini nikikujibu kulingana na maamuzi ninampenda sana, kwasababu nimeamua kumpenda. Mtu anayeingia kwenye mahusiano awe ni mtu anayefanya maamuzi na kuyasimamia.

## Kuitambua dhahabu katikati ya mchanga

Ni vizuri kufahamu ya kwamba dhahabu ni aina ya jiwe, ni mojawapo ya mawe. Tofauti ya dhahabu na mawe mengine ni kwamba, dhahabu inaitwa jiwe la thamani. Dhahabu inapatikana katikati ya mawe menzake, kwahiyo ukitaka dhahabu utaipata kwenye mawe. Na dhahabu inapatikana kwenye mfumo ghafi (raw-material) huwezi kukuta dhahabu iliyosafishwa katikati ya mawe, yaani unaenda mgodini halafu unaenda kukuta ile dhahabu safi imesafishwa vizuri ing'aa ukaikuta kwenye mawe. Ukienda mgodini utaikuta dhahabu kwenye mfumo ghafi. Muonekano wa dhahabu ghafi na muonekano wa dhahabu iliyosafishwa ni tofauti.

Kwasababu hiyo basi kuna uwezekano mkubwa sana wa kuiacha dhahabu ukiikuta kwenye mfumo wake ghafi. Ama ukaipuuza au usiijue, mpaka ufundishwe muonekano wa dhahabu. Watu wengi wakiambiwa wakaonyeshe dhahabu jinsi ilivyo hawajua kwasababu akili zinajua dhahabu ile dhahabu safi, haaitambui dhahabu ghafi. Watu wengi watapishana na dhahabu,

Kwa mfano huo ndivyo ilivyo ya kwamba wanawake na wanaume wenye sifa za kuoa na kuolewa katikati ya mawe menzao yaani katikati tu ya watu wengine. Sasa watu wengi wana picha ya mtu ambaye ameshatengezwa, wengi mnaangalizia waume na wake za watu ambao walishatengenezwa, na wewe kachimbe! Na ukija mgodini ni lazima utaona mawe mawe tu. Ukitumia sifa za mke wa mtu kutafuta wako sio rahisi kupata kwasababu wake za watu ni wameshatengezwa tayari, wewe unawaona kama dhahabu inayong'aa (pure gold) Lazima ujue uwe na mentality ya mchimbaji ndio uweze kwenda kuisort out katikati ya mawe.

Ukiangalia Waefeso 4:11-12. “Naye alitoa wengine kuwa mitume,na wengine kuwa manabii,na wengine kuwa

wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu;kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu,hata kazi ya huduma itendeke,hata mwili wa Kristo ujengwe" Anazungumzia Mungu alivyotoa wengine kuwa mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji na walimu, halafu mstari wa 12 anasema "kwa ajili ya kuwakamilisha watakatifu" Hawa watu wanaokamilishwa wanaitwa watakatifu, lakini wanahitaji kukamilishwa, sio kuwakamilisha wenye dhambi, ni watakatifu. Watakatifu wapo kwenye njia ya kukamilishwa na kwasababu hiyo kila ukitazama namna hii unaweza ukaona bado hajakamilika, kumbuka tu ya kuwa wote tupo kwenye mchakato wa kukamilishwa, kuna vitu havijakamilika kwenye maisha ya watu.

Hata wewe wenyewe upo kwenye mchakato wa kukamilika. Sifa ya kwanza ya Dhahabu ni, Anajifahamu na kujipambanua zaidi ya vipimo au viwango vya dunia. Dhahabu anaweza kusema mimi ni mweusimweusi lakini ninao uzuri. Anajifahamu, anaweza kujipaabanua, anaweza akasema kwa ujasiri kwamba mimi ni mzuri. Kwa namna anavyosema unaweza kujua ya kuwa hachukuliwi na upepo, hachukuliwi na fasheni,

hachukuliwi na mambo yanavyoenda, ni mtu ambaye anajifahamu. Na kujifahamu kwa kwanza ni kuokoka.

Kwahiyo mtu aliyeokoka tayari ameingia kwenye dhahabu. Mtu aliyeokoka, siyo anayeenda kanisani. Kwasababu hata mimi nimelelewa kwenye familia ambayo watu wameokoka wanampenda Yesu na mimi nimepelekwa sana kanisani, lakini nilikuwa bado sijaokoka, kwahiyo kuna wakati ambao nilifanya maamuzi ya kukoka mwenyewe.

Mtu ambaye viwango au vipimo vya uzuri vya dunia, viwango vya elimu vya elimu, viwango vya mafanikio dunia havimbebi, Mtu ambaye anajijua yeye ni nani. Ni mtu ambaye anajua anaenda wapi kwenye maisha.

Nimewahi kutoa mfano mmoja ya kwamba kuna mzee mmoja zamani kulikuwa na mashindano ya kulima na hayo mashindano unapolima kwa trekta uhakikishe umenyoosha mstari.Huyu ndugu alianza kushiriki mashindano akiwa kijana mpaka akawa mzee, miaka yote ni yeye tu anashinda. Wakati anastaafu wakamuuliza ni nini siri ya ushindi wako mfululizo. Akawajibu,

nlichokuwa nafanya nilikuwa nikikaa kwenye trekta ninatuma mtu aende mwisho wa shamba anaenda kuchomeka kijiti, na kazi yangu ninaanza kuipanga trekta lile bomba linalotoa moshi nahakikisha limeelekea kijiti, kwahiyo kazi yangu ni kuhakikisha bomba linalotoa moshi linaenda kukigonga kijiti ndio maana muda wote nilikuwa nalima bila kugeuka nyuma, lakini kuna wengine wanalima huku wanageuka nyuma.

Huu ni mfano mzuri wa mtu mwenye maono.Mtu anayejua mwisho wa shamba anaenda kugonga kijiti. Mtu anayejitambua anajua mwisho wa shamba ninaenda kugonga kijiti. Anajua mwisho wa maisha yake anatakiwa awe ameshakamilisha vitu gani. Kuna mtu hata hajui siku akiondoka duniani dunia ataiachia nini. Ndiyo hayo sasa marehemu ameaacha mume na watoto. Hivi unajua hata ngombe akichinjwa anaacha mke na watoto?

Ukisikia kijana anasema nikimaliza chuo niatajenga nyumba, hata ngombe ana zizi, hizo akili za kuwaza kuwa na sehemu ya kuishi ni akili za wanyama. Lazima uiachie dunia alama, hao ndio watu wanaojitambua. Anajua mwisho wa shamba kuna nini.

Mtu anayejitambua unagundua ana adabu, pasipo maono watu huacha kujizuia au tafsiri nyingine zinasema watu hupasua mipaka, au watu huvuka mipaka.

Maono yanakufunga unakuwa na adabu. Kwanini hauendi club? Sio tu kwasababu umeokoka ila ni kwa ajili ya mambo ambayo Mungu amekuandalia au unayaoyaendea kwenye maisha yangu, unajikuta unakosa hata muda wa kufanya hivyo. Kwanini kuna aina fulani ya marafiki huna? Kwasababu ya aina ya maisha uliyochagua. Kwanini unasoma kwa bidii? Ile wanasema mtu anasomea kijiji, hiyo ni kujishusha, waambie unasomea dunia sio tu kijiji. Biblia inasema "mimi ni nuru ya ulimwengu" ukiniambia nasomea kijiji ni kunikosea adabu. Lazima usome kwa ajili ya dunia.

Lazima uwe mtu unayejitambua ambaye atasema sasa ninaamka kuomba nakufanya vitu vyangu fulani kwa wakati fulani na akatimiza. Unaweza ukajiamsha mwenyewe kwenda kuomba? Kuomba ni nafasi ya upendeleo maana unaenda kuongea na mmiliki wa mbingu na nchi halafu unaringa. Mtu anayejitambua

anaweza kuzuia tamaa zake. Mtu anayeweza akasema siwezi kuingia kulala kama sijamaliza kazi fulani.

Dhahabu ni mtu anayejitambua, mtu mwenye nidhamu. Dunia inaweza ikawa inafurahia watu wamevaa nguo fulani lakini wewe unajua hakuna thamani yeyote kwenye hizo nguo. Ukijitengeneza vitu vitakuja, nawapa hinywila ya kwamba, Usihangaikie vitu, jitengeneze! Vitu huwa vinavutwa na vitakufuata. Kama huyo mtu hajitambui sio dhahabu ni mawe.

ii. Hufanya kazi kwa bidii kutwa nzima.

Na kwa kufanya kazi simaanishi anayefanya kazi nyingi. Kuna watu wana kazi nyingi sana na matokeo kidogo. Kwahiyo unaweza ukaona anatembea huku na kule ila ukiangalia alichofanya ni hamna chochote. Na mwenye tabia ya kuzungazunguka huku na huko ni shetani, Mungu akamuuliza umetoka wapi? nimetoka kuzungukazunguka huku na huko. Lazima uwe na vitu vinavyoshikika (matokeo). Mtu anayewaza na anataka kuanzisha vitu. Kuna mtu ambaye amelala tu, hajawahi kununua hata

kitabu, hajawahi kutafuta semina zinofundishwa ili akajifunze, yupo tu.

iii. Mtu anayeweza kujitoa

Wimbo ulio bora 1:6 Yule dada anasema "lakini shamba langu mwenyewe sikulilinda..” Kwa maana ya kwamba muda mwingi kuangalia shamba la mzabibu mpaka akashindwa kuwekeza kwenye mwili wake. Mtu ambaye anaweza kujitoa kwa ajili ya wengine, mtu anyeweza akadhabihu muda wake, mtu anayeweza akadhabihu usingizi..Maombi ya Alfajiri usifikiri ni kazi rahisi, lakini tunadhabihu usingizi. Kuamka usiku kuomba unadhabihu, mtu anayeweza kufanya vitu kwa kudhabihu huyo ni dhahabu. Mtu ambaye hajawahi kudhabihu chochote hiyo siyo dhahabu hilo ni jiwe. Mtu ambaye anaweza akaacha chakula sio usanii ya kwamba umefunga. Mtu anayeweza akatoa fedha kwa ajili ya wengine, mtu anayeweza akatoa muda wake kwa ajili ya wengine.

iv. utii

Wimbo ulio bora 1:6. Kaka zake wa kambo wamemuweka awe mlinzi, sio baba yake sio mama yake amewekwa na kaka zake. Huyu dada aliweza kukaa kwasababu alikuwa ni mtiifu. Na hapa uniruhusu niseme, anatambua mamlaka ya kuwa hawa ni kaka zangu wamesema neno natakiwa nitii. Ukisikia binti ambaye hawezi kumsikiliza mama yake, kaka kimbia bila kugeuka nyuma. Haijalishi ana nini, kimbia. Mtu ambaye hawezi kumsikiliza na kumheshimu mama yake hawezi kukusikiliza wewe. Mtu ambaye hatii mamlaka ya walio juu yake, hafai.

Ndani ya ndoa kuna vitu vingi, kuna vitu ambavyo vitahijati muende kwa wenye mamlaka, wenye mamlaka juu yake akiwa hawatambui na anaweza akabishana nao, je mtaenda kwa nani? Huyu dada alionewa lakini alikaa. Mtu ambaye hatambui viongozi kwenye fellowship kwamfano, kimbia. Mambo yakigeuka ndani ya ndoa mtakosa pa kwenda na kukosa watu wa kuwawajibisha na kuwaonya ya kuwa msifanye tena hivyo. Kama hakuna mtu anayeweza kumyoosha namna hiyo achana naye, hao

wanaitwa self made, yaani amejitengeneza mwenyewe, Utii unaweza kuuona jinsi anavyowasiliana na mamlakaukiona anahanngaika kuwasiliana na mamlaka hilo ni jiwe sio dhahabu.

Kuna watu wana mahusiano na watu ambao hawajaokoka, huwa nawasikitikia mtu ambaye hawezi kumheshimu Mungu hawezi kumheshimu mwanadamu. Mtu ambaye hamtambui Mungu hawezi kumtambua mwanadamu, kwahiyo kuwa makini sana.

Mtu ambaye hawajibiki kwa Mungu hawezi kuwajibika kwa mwanadamu. Huwezi kumuuliza kwanini umechelewa, akakujibu vizuri, utasikia anasema wewe ni nani? Unaniuliza kama nani? Unaliuliza ili iweje? Mtu ambaye anawajibika kwa Mungu unaweza ukamwambia jambo hili halipendezi mbele ya Mungu na akakuelewa, mtu wa namna hiyo moyo wake una hofu ya Mungu na anaweza akatubu. Angalia kaka ambaye ni mtii, usiangalie kaka ambaye ni chanzo cha magomvi, watu ambao siku zote wapo kinyume na mamlaka, hao watu sio sawasawa, kuwa makini sana.

v. Unyenyekevu

Unyenyekevu ni hali ya kufundishika. Huyo mtu mnaweza mkajadili ya kuwa hiki kitu sio sawasawa, mtu ambaye anaweza akaelekezwa. Kuna wadada ni wabishi, yaani kabla hujamaliza sentensi anakukatisha, kadada kanaujua mwisho kabla ya mwanzo achana nako. Na kuna wanaume ambao akiwa anaelekezwa hataki kuelekezwa. Chagua mtu ambaye anafundishika, mnaweza mkakaa mkajadili.

Yesu alipowagawia wanafunzi mkate walikataka kwenye mkate mmoja ili wajue ya kwamba tunategemeana. Yule anayedhani ya kwamba ameubeba mkate pekeyake achana naye. Mtu anatakiwa kujua ya kuwa nina kipisi cha mkate kwahiyo natakiwa kukaa kujifunza na kuwasilikiza wengine. Mtu ambaye kila kitu yeye anakosoa, hapana. Mnyenyekevu ni mtu anayeweza akaonywa, mtu anayeweza akaitwa akaambiwa hapana na kusema samahani sitarudia tena. Mtu anayeweza akapokea maelekezo.

Kwenye maisha kuna vitu tutajadili na kuna vitu vitahitaji maelekezo kwanza halafu maelezo yatafuata. Sasa kuna watu ambao hawapokei maelekezo, wanataka waambiwe kwanza kwanini.

Ukiziangalia hizo sifa kuna watu wanakuja kichwani mwako, watu hao mara nyingi huwa hauwachagui kwasababu Dhahabu imefunikwa na mchanga. Unawaza jinsi anavyovaa, akivaa anavaa shati la njano, suluari ya kijani na viatu vya bluu. Ni dhahabu ila imefunikwa na mchanga. Mchanga huwa unaondolewa, kuvaa anaweza akafundishwa, kutembea anaweza akafundishwa, kuweka nywele kunafundishika. Watu wengi sana huwa wanapishana na dhahabu.

Mimi ungeniona wakati mama mchungaji anasema ndio, usingenitamani. Nilikuwa sina uzuri wa kunitamani. Mimi nimejua kuvaa mkanda nikiwa chuoni, nilikuwa nachukua kamba za viatu ndio natumia kama mkanda. Mkanda wangu wa kwanza ni zawadi ya mama mchungaji. Kuvaa vizuri na kupangilia nguo pia nimefundishwa,

Watu wa namna hiyo mara nyingi wako kwenye ghafi, hawavutii. Inawezekana ni kwenye malezi aliyotoka, hajafundishwa kuvaa, au kupangilia maneno, namna ya kuongea. Wewe umeenda kutafuta wa "instagram" ambao ni mawe. Mungu amewaficha kwenye mchanga namna hiyo ili wengine wapite. Hiyo dhahabu ukiichukua ukaanza kuitengeneza ndio utangundua watu wengi wanaanza kuikimbilia. Sasa hivi Bwana ameisitiri.

# SURA YA TANO: NAMNA YA KUENDESHA MAHUSIANO

Kuna vitu vikubwa vitatu katika kujenga mahusiano. Ujenzi, ulinzi na usalama.

i. Ujenzi

Wimbo ulio bora 2:1 tukiangalia huyu ni dada anazungumza, “Mimi ni ua la uwandani,ni nyinyoro ya mabondeni” Ua la uwandani ni ua la kawaida. Huyu ni kaka anajibu katika mstari wa 2 “Kama nyinyoro kati ya miiba,kadhalika mpenzi wangu kati ya binti. Hizi lugha zinatumika kuonyesha ujenzi, dada bado ana mashaka sababu ya hao wadada wengine japokuwa anajijua yeye ni nani na huyo kaka anamjenga.

Namna ya kuanzisha mahusiano ni kuanza kwa kumjenga huyo mtu. Unamjenga kwa kuanza kutoa mchanga, unaanza kumuondosha vitu ambavyo haviko sawasawa. Na ujenzi mzuri ni ule wa kutokea ndani kwenda nje using’ang’anie tu aende “gym” sio vibaya lakini ni lazima aanzie kujengwa roho yake. Biblia inasema “Mpenzi naomba ufanikiwe katika mambo yako yote na kuwa na

afya yako, kama vile roho yako ifanikiwavyo" 3Yohana1:2 Sehemu ya kwanza ni roho, kwahiyo unapomjenga mtu anza kujenga roho yake. Kama ni uchumba au mahusiano yoyote ujenzi uanzie kwenye roho.

Mtu ambaye mnaingia kwenye mahusiano halafu anasababisha humpendi Mungu tena, huendi ibadani tena, anakusababisha unaingia dhambini huyo siyo mjenzi huyo ni mharibifu. Mahusiano ni ujenzi, yaani ukiingia kwenye mahusiano unajikuta unampenda Mungu zaidi, unaweza ukaomba zaidi, unaweza ukaabudu zaidi, unasoma neno zaidi. Mjenge huyo dada ajiamini, unamjenga ajithamini, unamjenga ajipende, ajione ni wa maana.

Kuna wanawake saa nyingine akiona kitu ulichokibeba anaogopa, muaminishe ya kwamba anaweza. Usimharibu mtu, usimsaidie shetani kumharibu mtu usimuangushe mtu dhambini. Dada ukiona mtu ananena kwa lugha kama kanisa la Koritho lakini mambo yake ni ya kukuangusha sio sahihi achana naye. Mtu sahihi ni yule anayekujenga, na atakujenga kutokea ndani kwenda nje.

Atajenga hali yako ya kiroho, nafsi yako. Sio anaanza kukwambia umevaaje, muone ukitembea kama unarudi nyuma, wewe humuoni dada fulani akivaa anachomekea. Ukiona hivyo ujue anakuharibu maana anaondoa hali ya kujiamini. Mtu anayekupenda anakujenga ujithamini na kujiona wa maana.Saa nyingine watu wametoka kwenye mazingira ya kukataliwa na kusemwa vibaya, mtu anayekaa na wewe na kukujenga ni sahihi kwako.Ukimjenga mtu atakulipa ujenzi, mtu ukimharibu atakuharibu. Kama mpo kwenye mahusiano kila mara unataka kumshikashika kiuno, itakula kwako.

ii. Ulinzi na usalama

Kumbuka wana wa mama yake walimweka kwenye shamba la mzabibu alinde, lakini tena anasema kwa huyu ndugu nimepata kivuli (I am protected). Kumbuka alipigwa na jua, halafu anasema niko salama. Hakikisha binti ajisikie salama akiwa na wewe, sio anajihisi kubakwa bakwa hivi. Hivi unajua kuna watu ukikaa nao karibu unajisikia hauko sawa tu, kwasababu ya matendo na lugha yao. Dada anapaswa kujisikia salama akiwa na

wewe. Ajue amekaa na mtu ambaye ni mume wake na utamlinda

Wanaume wa kweli hawafanyi hivyo, tunza huyo dada. Hata kama ikitokea mbele ya safari asije kuwa mke wako atakuheshimu na atasema "yule dada aliyeolewa na yule kaka, kaka ana raha sana" Kwasababu anajua ni kivuli. Lazima uwe kivuli mahali ambapo dada atasema naliketi kivulini mwake kwa fuaraha, nimekaa kwa kujiacha sio chonjo.Wadada kwenye hayo mahusiano kama huapati kivuli ondoka tu (sepa). Lazima uwe na furaha kwenye kivuli.

Wimbo ulio bora 2:4 “Akanileta mpaka nyumba ya karamu,Na bendera yake juu yangu ni Mapenzi”. Wimbo Ulio bora 7:1-17, Kuna mahali walienda uwandani, “akanileta mpaka nyumba ya karamu” Lazima ujue huu ni utamaduni wa kiyahudi, kulikuwa na nyumba wanaenda kufanyia karamu. Watoto wa Ayubu kuna sehemu walikuwa wanaenda kufanyia sherehe. Ni nyumba ambayo wanaingia watu walioheshimiwa. Tafsiri yake ni kwamba huyu mtu sio tu amejenga mahusiano yakabakia

kwake alimpeleka kumtambulisha kwa watu wa heshima, watu wa ndani, watu ambao wanaweza kumwajibiisha.

Wanaweza wakawa ni watu wa umri wake, wanaweza wakawa ni watu wa juu yake lakini ni watu wake wa ndani, ambao wakisema anasikia. Mahusiano yoyote hayapaswi kuendelea bila kuwa wazi, kwani yakiwa wazi sio dhambi. Mahusiano yanayofahamika yako salama, mahusiano ambayo hayafahamiki hayako salama. Yafanyeni mahusiano yajulikane, yakijulikana mnawajibishwa. Kama ni siri huyo mtu anaweza akafanya upuuzi huko nje na hamna mtu atamwajibisha. Mahusiano yakijulikana ni kwa faida yako. “Na bendera juu yangu”. Kwenye biblia ya kingereza imesema “banner”, kama ambavyo Mungu ni bendera ya ushindi wetu. Jehova Nissi. Hakikisha anakupeleka nyumba ya karamu lakini mwambie aweke bendera juu yako. Mahusiano yanapaswa yajulikane.

**Kuhusu Mwandishi:**
Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis “Tai”, Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *“Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari.”* [Habakuki 2:14]

**Kuhusu New Vine Church:**
Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz

**Mawasiliano na Mwandishi:**



**NEW VINE CHURCH** | **Dodoma**



New Vine Church limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa *(Mathayo 5:13 -14/Yoeli 2:2 - 11).*

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz



**Mahali tulipo:** Swaswa mkabala na geti la Waziri Mkuu, Dodoma mjini.

**Ratiba za Ibada**

**Alhamisi** Saa 11:15 jioni - saa 12:15 jioni
**Jumapili** Saa 3:00 asubuhi - saa 6:30 mchana

nvc_dodoma +255 754 917 764

# KUHUSU MWANDISHI



James Kalekwa ni amemwamini Yesu kuwa BWANA na Mwokozi wa maisha yake. Ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma


pastorjameskalekwa

+255 754 917 764

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

MchungajiJK

+255 754 917 764